

Siku ya Jumapili, wazazi wa Manu walimpa  koti nyekundu la kuzuia mvua.
"Mama, naweza kulivaa koti sasa?" Manu aliuliza.
"La hasha, mpendwa wangu, mvua iko karibu, lakini kwa leo mawingu hayako," Mama akasema



Siku ya Jumatatu jua lika angaza tele. "Inaweza nyesha leo, Mama?" Manu akauliza. "La hasha Manu, sio leo. Ukilivaa koti la kuzuia mvua kwa sasa utaonekana mcheshi!" Mama akasema.



Siku ya Jumanne, rangi ya anga ikawa samawati. "Mama, Lini matarajio yangu yatakamilika?" akauliza Manu. "Sio leo, mpendwa wangu, kuna wingu jeupe moja tu angani!" Mama akasema.



Siku ya Jumatano ikawa na joto mingi. "Mama, Mbona isinyeshe?" Manu akauliza. " Mwanangu, nafikiri itanyesha hivi karibuni. Pengine kabla haijafika mchana." Mama akasema.



Siku ya Alhamisi Manu alienda mandari. "Mama, Itakuwaje ikinyesha? Ninaweza chukua koti la kuzuia mvua?" Manu akauliza. "La hasha mpendwa wangu, haitanyesha leo. Hilo wingu ndogo nyeupe liko juu sana angani," Mama akasema.



Siku ya Ijumaa ilikuwa na mawingu mengi.
" Mama, inaweza nyesha leo?" Manu aliuliza kwa sauti ya juu.
"Inaweza, mpendwa wangu. Kuna mawingu nyeusi chini ya anga." Mama akasema.



Siku ya Jumamosi ikaanza kwa kishindo!

Badaboom!

" Mama, huo ni mngurumo wa radi nasikia? Inaweza nyesha hivi karibuni?" Manu akauliza.



Kisha baadaye, ikaanza kunyesha!
"Ooh, inanyesha, inanyesha," Manu aliimba,
akikimbia inje.